**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI**
**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**686** **VITENDO VYA KUJIFUNZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 3** **Jumatatu, 04 Mei 2015 mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.

3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja aina nne za mazingira ambayo yanaweza kuchangia ukuaji wa lugha kwa mtoto.

2. Bainisha mambo manne ambayo humsaidia mtoto kujifunza lugha kwa haraka anapofikia umri wa kati ya miaka mitano hadi sita.

3. Fafanua kwa kifupi mambo manne utakayofanya kwa ajili ya kumjengea mtoto stadi ya kusikiliza.

4. Chambua manufaa manne ya mtoto kuitikia katika tendo la ujifunzaji.

5. Ainisha mbinu nne utakazotumia ili kumjengea mtoto uwezo wa kuwasiliana.

6. Eleza kwa kifupi mambo manne utakayofanya ili kumjengea mtoto utayari wa kusoma kabla ya kuanza somo.

7. Fafanua kwa kifupi manufaa manne ya kutumia mbinu ya michezo katika ufundishaji wa watoto wadogo.

8. (a) Taja maneno manne yasiyo na silabi fungamano utakayotumia kumfundisha mtoto matamshi.

   (b) Fafanua kwa kifupi maana ya dhana "kuitikia" katika tendo la ujifunzaji na ufundishaji wa mtoto.

9. Ainisha njia nne ambazo mtoto anaweza kuzitumia kujifunza lugha kutoka kwa watoto wenzake.

10. Bainisha kwa ufupi matendo manne ambayo mwalimu anaweza kuyafanya darasani ili kumwezesha mtoto kujua dhana ya mawasiliano.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza manufaa manne ya kurekebisha mara moja makosa ya usomaji wa neno au maneno kwa mtoto.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

12. Chambua na eleza mambo matano yanayoweza kumuathiri mtoto anapojifunza Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.

13. Bainisha changamoto tano wanazokutana nazo watoto katika kujifunza kuandika.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

14. Fafanua hatua tano utakazofuata ili kuwaongoza watoto kutambua herufi "a".

15. Bainisha faida tano za kutumia vifaa halisi unapomwongoza mtoto kujifunza kuandika katika hatua za mwanzo.

16. Eleza faida tano za kutumia mbinu ya vitendo katika ufundishaji wa lugha kwa watoto.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org